BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi na Nne – Tarehe 01 Juni, 2024**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:

247. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tathmini iko vipi juu ya tafiti za mienendo ya mifumo ya ikolojia na changamoto za kimazingira kwa sasa.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

54. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Tunaipongeza Serikali kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo kwa wajasiriamali.

(a) Je, ni vikundi vingapi vimepatiwa mkopo katika jimbo la Konde na viko wapi.

(b) Kwa kuwa kuna mikopo ya boda boda na ya mtu mmoja mmoja, je, ni boda boda ngapi zimetolewa na watu wangapi wamepatiwa mikopo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

93. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taasisi nyingi zinakabiliwa na changamoto ya kuwa na magari ambayo hayafanyi kazi na yanahitaji kuondolewa (disposal), hali inayochangia matumizi makubwa ya fedha za umma. Changamoto hii inatokana sana na upungufu wa matengenezo ya mara kwa mara kwa magari hayo, ambayo hupelekea kuuzwa kwa bei ndogo.

(a) Je, Serikali inatambua uzito wa tatizo hili na ni mkakati upi inauchukua kutatua suala hili ambalo linagharimu fedha nyingi za Serikali.

(b) Je, tathmini inaonesha ni idadi gani ya magari mabovu katika taasisi za umma hadi sasa na ni gharama ya kiasi gani Serikali huingia katika matengenezo.

(c) Je, Serikali ina mpango wa kuimarisha mikakati ya matengenezo ili kuhakikisha kuwa magari yanadumu kwa muda mrefu na kupunguza gharama za muda mrefu za ukarabati.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

196. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni lini Wizara yako itakamilisha ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya kujenga kiwanja cha mpira ndani ya jimbo la Mwanakwerekwe.

**Wizara ya Afya:**

80. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna taarifa kuwa Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa inakabiliwa na uhaba wa rasilimali watu, ikiwa ni pamoja na Wafamasia, Fundi Sanifu dawa, Afisa Tehama, Afisa Manunuzi, Mkaguzi wa Ndani na Wanasheria.

(a) Vipi Wizara yako inaifahamu taarifa hii.

(b) Ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi wanaohitaji huduma ya Wakala huyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

182. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kipindi kirefu nchi yetu imekumbwa na changamoto ya kuwa na uhaba wa walimu wenye uwezo, mbinu stadi na hata maarifa ya kufundisha somo la 'Literature'.

Je, Wizara inafanya jitihada gani katika kuhakikisha tunakuwa na walimu mahiri na wenye uzoefu wa kufundisha 'Literature' kwa lugha ya Kingereza.

188. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hakuna anaepinga kuwa walimu ni kada inayohangaika sana na maisha baada ya kustaafu.

Je, lini Serikali itafikiria utaratibu mzuri zaidi wa kuwaondoshea walimu kadhia hii ikiwemo kuwaongezea kima cha kustaafu.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

254. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali kwa kuiboresha miundombinu ya mawasiliano ikiwemo minara ya simu. Hata hivyo bado lipo tatizo la baadhi ya minara kutokuwa na taa, jambo ambalo linahatarisha usalama wa wananchi na mali zao.

Je, kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu jambo hilo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

199. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe):
Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazopata fursa ya kushirki kwenye mikutano ya kitaifa na kimataifa kwenye mifumo ya chakula barani Afrika.

Ni faida gani ambazo Zanzibar inazipata katika ushiriki huo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

149. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Hivi karibuni kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani, tumeshuhudia tatizo la kukosekana kwa huduma ya umeme katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, jambo ambalo lilipelekea usumbufu pamoja na khofu kubwa kwa wananchi wetu. Kwa kuwa nishati ya umeme ni jambo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yoyote ile.

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani kuhusiana na zoezi la kupatikana kwa nishati mbadala ya umeme hapa Zanzibar.

(b) Je, ni ipi kauli hasa ya Serikali katika jambo hili.

(c) Je, Serikali haioni kuwa haiwezi kuwa na uwekezaji madhubuti bila ya kuwepo nishati ya uhakika ya umeme hapa Zanzibar.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
01 Juni, 2024.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA